09

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR,

# SEPTEMBA, 2024

Funded by the European Union

18 OKTOBA, 2024

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA SEPTEMBA, 2024

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukioyaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).

## LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji na watunga sera pamoja na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Septemba, 2024 ambapo waathirika walikuwa 148. Waathirika wengi walikuwa watoto (miaka 0 -17) sawa na asilimia 87.9, wanawake(miaka 18 au zaidi) asilimia 7.4 na wanaume(miaka 18 au zaidi) asilimia 4.7.


Miongoni mwa watoto (waathirika 130), wasichana walikuwa 107 (asilimia 82.3) na wavulana walikuwa 23 (asilimia 17.7).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Septemba 2024**



Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 64, ambapo waathirika 62 walikuwa wasichana na wawili(2) walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 15 ambapo waathirika 14 walikuwa wavulana na mmoja(1) alikuwa mwanamme. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni sita (6) ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha ni tisa (9) ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 28 kati ya hayo waathirika 23 walikuwa wasichana, manne(4) walikuwa wanawake na mmoja (1) alikuwa mvulana. Matukio ya shambulio yalikuwa 26 ambapo waathirika saba (7 ) walikuwa wasichana, nane(8) walikuwa wavulana, watano(5) walikuwa wanawake na sita (6) walikuwa wanaume.


**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio, Septemba, 2024**




Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 41) sawa na asilimia 27.7 ikifuatia wilaya ya Magharibi "B" ambapo yameripotiwa matukio 37 (asilimia 25.0).

Wilaya ya Wete, Micheweni na Mkoani zimeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio matatu (3) yameripotiwa sawa na asilimia 2.0 kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Septemba, 2024**




Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 5.7 kufikia matukio 148 mwezi wa Septemba, 2024 kutoka matukio 157 kwa mwezi wa Agosti, 2024. Aidha, matukio ya shambulio, shambulio la aibu/Kukashifu na kulawiti/kunajisi yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Septemba 2024.

Wilaya ya Magahribi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya nyengine (matukio 41) kwa mwezi wa Septemba, 2024 na wilaya ya Magahribi "A" pia iliongoza kwa mwezi wa Agosti , 2024 (matukio 38).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Agosti, 2024 na Septemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Agosti 2024 | Sept 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 |
| Kaskazini 'A' | 10 | 6 | 7 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 6 | 1 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 11 | 7 | 7 | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 5 | 2 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Mjini | 31 | 27 | 19 | 7 | 0 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 2 | 4 | 7 | 11 |
| Magharibi 'A' | 38 | 41 | 17 | 16 | 4 | 3 | 2 | 2 | 5 | 3 | 5 | 8 | 5 | 9 |
| Magharibi 'B' | 33 | 37 | 18 | 17 | 3 | 3 | 3 | 2 | 1 | 0 | 4 | 9 | 4 | 6 |
| Wete | 5 | 3 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 12 | 10 | 2 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 5 | 2 | 5 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 7 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **157** | **148** | **80** | **64** | **14** | **15** | **7** | **6** | **16** | **9** | **24** | **28** | **16** | **26** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 5.7 kufikia matukio 148 kwa mwezi Septemba, 2024 kutoka matukio 157 kwa mwezi wa Septemba, 2023. Ambapo matukio ya Kutorosha na Shambulio yameripotiwa kupungua kwa mwezi Septemba, 2024. Wilaya ya Magharibi “A” imeongoza kwa idadi kubwa na idadi sawa ya matukio kwa Septemba, 2024 na Septemba, 2023 (matukio 41 kwa kila mwezi).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Septemba 2023 na Septemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 |
| Kaskazini 'A' | 8 | 6 | 1 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 5 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 6 | 4 | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 |
| Kati | 6 | 7 | 2 | 4 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini | 7 | 5 | 5 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Mjini | 32 | 27 | 10 | 7 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 1 | 4 | 4 | 15 | 11 |
| Magharibi 'A' | 41 | 41 | 19 | 16 | 3 | 3 | 1 | 2 | 5 | 3 | 2 | 8 | 11 | 9 |
| Magharibi 'B' | 29 | 37 | 9 | 17 | 4 | 3 | 2 | 2 | 1 | 0 | 4 | 9 | 9 | 6 |
| Wete | 7 | 3 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 3 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 10 | 4 | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **157** | **148** | **59** | **64** | **15** | **15** | **6** | **6** | **11** | **9** | **24** | **28** | **42** | **26** |

Miongoni mwa watoto 130 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 62, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 14, Kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana sita(6), Kutorosha walikuwa wasichana tisa(9), shambulio la aibu/kukashifu walikuwa 24 ambapo 23 walikuwa wasichana na mmoja(1) alikuwa mvulana na shambulio walikuwa 15 kati yao wasichana walikuwa saba(7) na wavulana walikuwa nane(8).

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Septemba, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 6 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 6 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 7 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 4 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 20 | 7 | 2 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 | 2 | 3 |
| Magharibi 'A' | 36 | 16 | 2 | 2 | 3 | 0 | 7 | 0 | 3 | 3 |
| Magharibi 'B' | 32 | 15 | 3 | 2 | 0 | 0 | 8 | 0 | 2 | 2 |
| Wete | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 5 | 1 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 3 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **130** | **62** | **14** | **6** | **9** | **0** | **23** | **1** | **7** | **8** |

Miongoni mwa wanawake 11 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa wawili(2), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wanane (4) na shambulio walikuwa wanawake watano (5).

**Jadweli 1.4a: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Septemba, 2024**

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | Idadi ya Waathirika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 4 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 4 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **2** | **0** | **0** | **4** | **5** | **11** |

Miongoni mwa wanaume saba (7) walioripotiwa kufanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, mwanamme alielawitiwa alikuwa mmoja(1) na sita (6) walifanyiwa shambulio.

**Jadweli 1.4b: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Septemba, 2024**

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | Iddai ya Waathirika |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio | |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 3 | 4 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **1** | **0** | **0** | **6** | **11** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya ukatili na udhalilishaji (matukio 67) sawa na asilimia 51.5 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 32) sawa na asilimia 24.6. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 44) sawa na asilimia 71.0 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Idadi ya Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Septemba, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Idadi ya Waathirika |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 1 | 2 | | | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 7 |
| 6-10 | | 4 | 5 | | | 2 | 0 | 0 | 0 | 10 | 1 | 2 | 24 |
| 11-14 | | 13 | 5 | | | 2 | 0 | 0 | 1 | 6 | 3 | 2 | 32 |
| 15-17 | | 44 | 2 | | | 1 | 0 | 9 | 0 | 4 | 4 | 3 | 67 |
| **Jumla** | | **62** | **14** | | | **6** | **0** | **9** | **1** | **23** | **8** | **7** | **130** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Septemba, 2024 yamepungua kwa asilimia 5.1 kufikia matukio 130 kwa mwezi wa Septemba 2024 kutoka 137 kwa mwezi wa Agosti 2024. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa miaka 0-5, 6-10 na 11-14 yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Septemba 2024.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Idadi ya Waaathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Agosti 2024 na Septemba 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Idadi ya Waathirika | |
| | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 |
| 0-5 | 2 | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 | 0 | 6 | 7 |
| 06-10 | 2 | 4 | 7 | 5 | 0 | 2 | 1 | 0 | 9 | 10 | 0 | 3 | 19 | 24 |
| 11-14 | 12 | 13 | 5 | 5 | 3 | 2 | 3 | 0 | 4 | 7 | 4 | 5 | 31 | 32 |
| 15-17 | 55 | 44 | 1 | 2 | 2 | 1 | 11 | 9 | 4 | 4 | 8 | 7 | 81 | 67 |
| **Jumla** | **71** | **62** | **14** | **14** | **5** | **6** | **15** | **9** | **20** | **24** | **12** | **15** | **137** | **130** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 6.6 kufikia matukio 130 kwa mwezi wa Septemba 2024 kutoka matukio 122 kwa mwezi wa Septemba 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Septemba , 2024.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Septemba, 2023 na Septemba, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Idadi ya Waathirika | |
| | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 |
| 0-5 | 6 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 6 | 3 | 0 | 0 | 14 | 7 |
| 6-10 | 8 | 4 | 9 | 5 | 0 | 2 | 0 | 0 | 7 | 10 | 1 | 3 | 25 | 24 |
| 11-14 | 17 | 13 | 4 | 5 | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 7 | 11 | 5 | 39 | 32 |
| 15-17 | 21 | 44 | 0 | 2 | 0 | 1 | 9 | 9 | 3 | 4 | 11 | 7 | 44 | 67 |
| **Jumla** | **52** | **62** | **15** | **14** | **5** | **6** | **11** | **9** | **16** | **24** | **23** | **15** | **122** | **130** |

Matukio mengi (matukio 64) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 43.2 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea sehemu nyengine (matukio 46) sawa na asilimia 31.1 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Septemba, 2024**





Matukio 112 kati ya matukio 148 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 75.7, matukio 31 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 20.9 ,matukio 2 yamefungwa na polisi( asilimia 1.4 ) na matukio 3 yapo mahakamani sawa na asilimia 2.0.

**Jadweli 1.8: Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Septemba, 2024**

| | | Waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji | | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya makosa | Idadi ya makosa | Watu wazima | | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi |
| | | Wanaume | Wanawake | M'me | M'ke | | | | | | |
| Kubaka | 64 | | 2 | | 62 | 3 | 0 | 0 | 2 | 14 | 45 |
| Kulawiti/Kunajis | 15 | 1 | | 14 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 12 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 6 | | 0 | | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 |
| Kutorosha | 9 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 28 | 0 | 4 | 1 | 23 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 23 |
| Shambulio | 26 | 6 | 5 | 8 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 21 |
| **Jumla** | **148** | **7** | **11** | **23** | **107** | **3** | **0** | **0** | **2** | **31** | **112** |

Waliofanya matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Septemba 2024 walikuwa 148 kati yao, 111 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 75.0 , jirani walikuwa 35 sawa na asilimia 23.6 na wawili (2) walikuwa wapenzi 1.4.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Septemba, 2024**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR SEPTEMBA, 2024

Jumla ya Majalada 96 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Septemba, 2024 ambayo yalihusisha makosa 102.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 67) sawa na asilimia 65.7 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Septemba,2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 2 | 2 |
| Kusini Unguja | 14 | 14 |
| Mjini Magharibi | 63 | 67 |
| Kaskazini Pemba | 8 | 8 |
| Kusini Pemba | 9 | 11 |
| Makao Makuu | 0 | 0 |
| **Jumla** | **96** | **102** |

Kati ya Majalada 96 yaliyopokelewa, majalada 17 yamependekezwa kufungwa, majalada 29 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 31 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada 19 hayajatolewa uamuzi.

**Jadweli 2.2: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Septemba 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalio ruhusiwa kwenda Mahakamani | Yalio Pendekezwa kufungwa | Yalio rudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kusini Unguja | 14 | 8 | 1 | 3 | 2 |
| Mjini Magharibi | 63 | 11 | 13 | 23 | 16 |
| Kaskazini Pemba | 8 | 6 | 0 | 2 | 0 |
| Kusini Pemba | 9 | 6 | 3 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **96** | **31** | **17** | **29** | **19** |

Miongoni mwa makosa 102 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 62) sawa na asilimia 60.8 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Septemba 2024**

| Aina ya Mkosa | Idadi ya Makosa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Makao Makuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 62 | 2 | 6 | 45 | 5 | 4 | 0 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 8 | 0 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 |
| Kulawiti/Kunajis | 11 | 0 | 2 | 6 | 2 | 1 | 0 |
| Kutorosha | 6 | 0 | 0 | 3 | 1 | 2 | 0 |
| Shanbulio la Aibu/Kukashifu | 12 | 0 | 5 | 4 | 0 | 3 | 0 |
| Kubaka kwa kundi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kurusha picha za ngongo mtandaoni | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Ukatili wa Mtoto | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **102** | **2** | **14** | **67** | **8** | **11** | **0** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA SEPTEMBA 2024

Jumla ya mashauri 28 yamefunguliwa katika mahkama za udhalilishaji kwa mwezi wa Septemba, 2024 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 12) sawa na asilimia 42.9 ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Septemba, 2024**




Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika mahkama za udhalilishaji Zanzibar ni 28, ambapo mashauri matatu (3) yamepatiwa uamuzi na mashauri 25 bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Makosa Septemba, 2024**

| Aina ya Kosa | Zilizofunguliwa | Zilizotolewa uamuzi | | | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Huru | Kufutwa | Faini | |
| Kubaka | 19 | 0 | 1 | 2 | 16 |
| Kulawiti | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kutorosha | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Kumuingilia maharimu | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **28** | **0** | **1** | **2** | **25** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 28 ambapo washtakiwa wote walikuwa wanaume. Washtakiwa wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 18-21 (washtakiwa 7) sawa na asilimia 25.0

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 28 ambapo muathirika mmoja (1) alikuwa mwanamme na waathirika 27 walikuwa wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 15-19 (waathirika 15) sawa na asilimia 53.6.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Septemba, 2024**


| Umri wa Mshtakiwa | Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| 14-17 | 6 | 0 | 0-4 | 0 | 0 |
| 18-21 | 7 | 0 | 5-9 | 0 | 7 |
| 22-25 | 6 | 0 | 10-14 | 0 | 5 |
| 26-29 | 3 | 0 | 15-19 | 1 | 14 |
| 30-33 | 3 | 0 | 20-24 | 0 | 1 |
| 34-37 | 3 | 0 | 25-29 | 0 | 0 |
| 38-41 | 0 | 0 | 30-34 | 0 | 0 |
| 42-45 | 0 | 0 | 35-39 | 0 | 0 |
| 46-49 | 0 | 0 | 40-49 | 0 | 0 |
| 50+ | 0 | 0 | 50+ | 0 | 0 |
| **Jumla** | **28** | **0** | **Jumla** | **1** | **27** |

## WANAFUNZI NA MAHABUSU WA MAKOSA YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA WA CHUO CHA MAFUNZO

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya udhalilishaji waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Julai -Septemba, 2024 walikuwa 32 na Mahabusu walikuwa 123.


Wilaya ya Mjini imeripotiwa kupokea wanafunzi na mahabusu wengi ukilinganisha na wilaya nyengine, wanafunzi 11 na mahabusu 41.

**Kielelezo 4.1: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya, Julai - Septemba, 2024**




Umri wa miaka 30-39 umeripotiwa kuwa na wanafunzi wengi zaidi (wanafunzi 10) ikilinganishwa na umri mwengine. Aidha, kwa upande wa mahabusu, idadi kubwa pia imeripotiwa katika umri wa miaka 30-39 (mahabusu 35).

**Kielelezo 4.2: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri, Julai - Septemba 2024**




Wanafunzi wengi wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 11 na zaidi (wanafunzi 12) sawa na asilimia 37.5 ikilinganishwa na muda mwengine wa kutumikia vifungo .

**Jadweli 4.3: Idadi ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kwa Muda wa Vifungo na Aina ya Makosa, Julai - Septemba, 2024**

| Muda wa kutumikia kifungo Chuoni (Gerezani) | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | kujaribu kubaka | Kulawiti | Kujaribu kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | Kuingilia magharimu | |
| Chini ya miezi 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miezi 4-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Mwaka 1-2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 4 |
| Miaka 3-5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 6 |
| Miaka 6-10 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 4 | 1 | 8 |
| Miaka 11+ | 6 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 |
| **Jumla** | **6** | **1** | **4** | **1** | **2** | **3** | **6** | **8** | **1** | **32** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Septemba, 2024 ambapo waathirika walikuwa 148. Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 41) sawa na asilimia 27.7. Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 5.7 kufikia matukio 148 mwezi wa Septemba, 2024 kutoka matukio 157 kwa mwezi wa Agosti, 2024.

Matukio 112 kati ya matukio 148 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 75.7, matukio 31 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 20.9 ,matukio 2 yamefungwa na polisi( asilimia 1.4 ) na matukio 3 yapo mahakamani sawa na asilimia 2.0.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Septemba, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 3 | 3 | 6 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 25 | [redacted] | 25 | [redacted] | 6 | 6 | 3 | [redacted] | 3 | 7 | 0 | 7 | 11 | 1 | 12 | 5 | 6 | 11 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 4 | [redacted] | 4 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 13 | [redacted] | 13 | [redacted] | 2 | 2 | 3 | [redacted] | 3 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 1 | 1 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 22 | [redacted] | 22 | [redacted] | 7 | 7 | 0 | [redacted] | 0 | 1 | 0 | 1 | 8 | 0 | 8 | 4 | 4 | 8 |
| **Jumla** | **64** | [redacted] | **64** | [redacted] | **15** | **15** | **6** | [redacted] | **6** | **9** | **0** | **9** | **27** | **1** | **28** | **12** | **14** | **26** |

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio baina ya Mwezi Agosti, 2024 na Septemba, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Idadi | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Sept 2024 |
| Nyumbani kwa Muathirika | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 6 | 6 | 10 | 9 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 30 | 25 | 4 | 6 | 3 | 3 | 9 | 7 | 8 | 12 | 7 | 11 | 61 | 64 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 6 | 4 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 9 | 6 |
| Sehemu za kazi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 19 | 13 | 4 | 2 | 0 | 3 | 1 | 0 | 5 | 4 | 0 | 1 | 29 | 23 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 22 | 22 | 5 | 7 | 2 | 0 | 6 | 1 | 10 | 8 | 3 | 8 | 48 | 46 |
| **Jumla** | **80** | **64** | **14** | **15** | **7** | **6** | **16** | **9** | **24** | **28** | **16** | **26** | **157** | **148** |

Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Septemba, 2024

| Wilaya | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | Idadi ya Matukio |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| Kaskazini 'A' | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 6 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| Kati | 4 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 7 |
| Kusini | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 5 |
| Mjini | 7 | 2 | 2 | 1 | 4 | 11 | 27 |
| Magharibi 'A' | 16 | 3 | 2 | 3 | 8 | 9 | 41 |
| Magharibi 'B' | 17 | 3 | 2 | 0 | 9 | 6 | 37 |
| Wete | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 |
| Chake Chake | 5 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 10 |
| Mkoani | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 |
| **Zanzibar** | **64** | **15** | **6** | **9** | **28** | **26** | **148** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Agosti, 2024 na Septemba, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 | Agosti 2024 | Septemba 2024 |
| Kubaka | 80 | 64 | 9 | 2 | 71 | 62 | | | | |
| Kulawiti | 14 | 15 | | | | | 14 | 14 | 0 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 7 | 6 | 2 | 0 | 5 | 6 | | | | |
| Kutorosha | 16 | 9 | 1 | 0 | 15 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 24 | 28 | 4 | 4 | 15 | 23 | 5 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 16 | 26 | 2 | 5 | 6 | 7 | 6 | 8 | 2 | 6 |
| **Jumla** | **157** | **148** | **18** | **11** | **112** | **107** | **25** | **23** | **2** | **7** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Septemba, 2023 na Septemba, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 | Sept 2023 | Sept 2024 |
| Kubaka | 59 | 64 | 7 | 2 | 52 | 62 | | | | |
| Kulawiti | 15 | 15 | | | | | 15 | 14 | 0 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 6 | 1 | 0 | 5 | 6 | | | | |
| Kutorosha | 11 | 9 | 0 | 0 | 11 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 24 | 28 | 8 | 4 | 14 | 23 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 42 | 26 | 12 | 5 | 11 | 7 | 12 | 8 | 7 | 6 |
| **Jumla** | **157** | **148** | **28** | **11** | **93** | **107** | **29** | **23** | **7** | **7** |

**Jadweli 5.0: Idadi ya Waathirika Wanawake wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Septemba 2024**

| Umri | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | Idai ya Waathirika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| 18-29 | 2 | 0 | 0 | 3 | 4 | 9 |
| 30-39 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| 40-49 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 50-59 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **0** | **4** | **5** | **11** |

**Jadweli 6.0: Idadi ya Waathirika Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Septemba 2024**

| Umri | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | Idadi ya Waathirika |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| 18-29 | 1 | 0 | 0 | 6 | 7 |
| 30-39 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 40-49 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 50-59 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **1** | **0** | **0** | **6** | 7 |

**Jadweli 7.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea; Septemba, 2024**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 4 | 1 | 0 | 0 | 4 | 2 | 11 |
| 03:01 - 6:00 Mchana | 7 | 3 | 0 | 1 | 5 | 5 | 21 |
| 6:01 - 9:00 Jioni | 11 | 3 | 1 | 2 | 7 | 3 | 27 |
| 9:01 - 12:00 Jioni | 16 | 5 | 1 | 3 | 6 | 5 | 36 |
| 12:01 - 3:00 usiku | 23 | 3 | 3 | 3 | 6 | 7 | 45 |
| 3:01 - 6:00 Usiku | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 8 |
| 6:01 - 09:00 Usiku | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **64** | **15** | **6** | **9** | **28** | **26** | **148** |

**Jadweli 8: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Miezi na Wilaya, 2024**

| Miezi | Kaskazini 'A' | Kaskazini 'B' | Kati | Kusini | Mjini | Magharibi 'A' | Magharibi 'B' | Wete | Micheweni | Chake Chake | Mkoani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 5 | 7 | 5 | 1 | 43 | 33 | 47 | 3 | 6 | 20 | 1 | 171 |
| Februari | 4 | 13 | 8 | 5 | 39 | 39 | 43 | 8 | 2 | 9 | 5 | 175 |
| Machi | 4 | 5 | 6 | 1 | 25 | 38 | 34 | 6 | 0 | 4 | 2 | 125 |
| Aprili | 3 | 2 | 11 | 1 | 34 | 40 | 31 | 10 | 3 | 10 | 3 | 148 |
| Mei | 4 | 9 | 10 | 4 | 45 | 37 | 34 | 8 | 4 | 10 | 7 | 172 |
| Juni | 5 | 6 | 12 | 7 | 36 | 48 | 38 | 5 | 9 | 4 | 4 | 174 |
| Julai | 3 | 6 | 8 | 5 | 32 | 28 | 52 | 8 | 7 | 9 | 7 | 165 |
| Agosti | 10 | 5 | 11 | 3 | 31 | 38 | 33 | 5 | 2 | 12 | 7 | 157 |
| Septemba | 6 | 6 | 7 | 5 | 27 | 41 | 37 | 3 | 3 | 10 | 3 | 148 |
| Oktoba | | | | | | | | | | | | |
| Novemba | | | | | | | | | | | | |
| Disemba | | | | | | | | | | | | |
| **Jumla** | **44** | **59** | **78** | **32** | **312** | **342** | **349** | **56** | **36** | **88** | **39** | **1,435** |

**Jadweli 9: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Miezi , 2020-2024**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 116 | 122 | 65 | 173 | 171 |
| Februari | 155 | 100 | 100 | 164 | 175 |
| Machi | 136 | 141 | 82 | 155 | 125 |
| Aprili | 95 | 108 | 68 | 148 | 148 |
| Mei | 118 | 66 | 74 | 154 | 172 |
| Juni | 102 | 97 | 97 | 127 | 174 |
| Julai | 114 | 108 | 78 | 168 | 165 |
| Agosti | 116 | 96 | 131 | 175 | 157 |
| Septemba | 115 | 90 | 170 | 157 | 148 |
| Oktoba | 103 | 107 | 164 | 199 | |
| Novemba | 92 | 90 | 177 | 172 | |
| Disemba | 101 | 97 | 154 | 162 | |
| **Jumla** | **1,363** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,435** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
MMP, Zanzibar.